SHINDANO LA INSHA: Jinsi Femina HIP ilivyobadili maisha yangu.

Mshindi namba 1: Christine Peter Bisangwa, Dar es Salaam.

Jarida la Fema, nilianza kulifahamu mwaka 2000 nilipokuwa kidato cha kwanza. Liliitwa Femina. Sikuweza kumudu kununua jarida hivyo nilifaidika kulisoma aidha kwa kwenda maktaba ya shule au kuazima kwa wanafunzi waliopata nakala. Ndio ukawa utaratibu wa maisha pale Kibasila Sekondari hadi nilipomaliza kidato cha nne. Baada ya kujiunga na kidato cha tano sikupata nafasi ya kulipata jarida kwani shule niliyosoma haikuwa na maktaba. Hivyo majarida ya Fema yakifika hapakuwa na sehemu maalum ya kusema mwanafunzi akasome labda kwa kubahatisha tu endapo utamwona mwalimu analo ndipo akuazime ukasome. Nilitumia muda wa likizo kutafuta majarida yaliyotoka ila sikupata yote hivyo kukosa baadhi ya matoleo.

Jarida la Fema limebadilisha maisha yangu kwa kiwango kikubwa sana katika sehemu zifuatazo;

Kijamii, jarida lilinisaidia sana katika kuanzisha uhusiano wa kimapenzi, nilianza nikiwa na zaidi ya miaka 18, limenisaidia kuvuka salama katika kipindi cha mpito (foolish age), majibu ya 'Mpendwa anti" kwa maswali ya wasomaji yamenisaidia sana na kuniwezesha kukua salama. Jarida la Fema limenijenga sana na kunisaidia kuwa na uhusiano mzuri na wanajamii. Pia limenijengea ujasiri wa kuzungumza na watu mbalimbali kuhusu mahusiano na VVU. Kupitia kurasa za "Dear Anko" nimepata kujifunza mambo mengi yanayotokea katika jamii zetu kama vile Ndumba za mapenzi, Kidume cha Mademu, Msafiri kafiri na Samaki pande mbili. Jarida la femina January-March 2006, Anko Charles alizungumzia jambo ambalo nililisikia tu, alinifumbua macho zaidi pale alipokwenda kwa daktari na kumweleza faida na athari za kumgeuza samaki. Kwa hiyo hili linaniweka makini kuweza kujadili na vijana wenzangu kuhusu madhara ya kumgeuza samaki.

Jarida limenisaidia sana kunijengea self confidence. Kwani kwa sasa naweza kusimama na kujieleza kwa makini bila ya kuona woga. Zamani sikuweza kudiriki kumwambia daktari kwamba nina muwasho sehemu za siri kwa kudhani kuwa atafikiri nimefanya ngono, hivyo ikawa nanunua dawa mwenyewe na kujitibu. Lakini kupitia Fema limenijengea ujasiri ambao naweza nikasema chochote bila ya kumwofia yoyote, nikiwa kwenye hedhi nikihitaji pad kama nitaenda dukani na kukuta muuzaji wa kiume siwezi kununua nitaenda kutafuta duka analouza mwanamke na kama ningekuta watu wengine ningesubiri hadi waishe ndipo niseme kile ninachokihitaji sikujiamini, kupitia

jarida la Fema sasa ninaweza kwenda dukani si kununua tu pad bali naweza hata kununua condom bila kujali chochote.

Kufahamu mila na desturi za jamii nyingine, jarida la Fema limefanya katika maisha yangu. Jarida limeniwezesha kufahamu mambo mengi yaliyopo hapa nchini ambayo nisingeweza kuyafahamu kwa undani bila ya kusoma Fema. January-March 2006, katika kurasa za ujinsia na mahusiano, jarida lilielezea kuhusu "Somo" ambae ni maarufu zaidi kwa mila za Zanzibar. Kabla sikujua chochote kuhusu Somo hadi niliposoma jarida hilo na kugundua kuwa Somo ni mwanamke anayechaguliwa ili kumwosha damu mwali na kumfunda pale anapovunja ungo, pia nimejifunza kwa undani na mifano zaidi madhara ya mimba na kuolewa katika umri mdogo.

Kielimu, Kusoma kwa bidii katika maisha yangu ya shule kulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kusoma majarida ya Fema. Kwa ujumla naweza kusema 25% ya kufaulu masomo yangu ya sekondari hadi kufikia Chuo Kikuu kulichangiwa na jinsi jarida la Femina/Fema linavyosisitiza vijana kupenda elimu. Mfano kupitia kurasa za Dear Aunt niliweza kuongeza juhudi za kujisomea kwani ushauri wake mkubwa kwa wote waliomuuliza maswali ni kuacha mambo yote mabaya katika umri mdogo na kukazania masomo. Hiyo ilinipa moyo zaidi nami kuendelea kusoma kwa bidii.

Sikuwa na tabia ya kujisomea mbali nay yale niliyojifunza darasani, lakini makala ya ‘Hatusomi lakini tusome nini?’ ilinivutia kusoma zaidi kwa kujiburudisha na kukuza upeo wangu. Nilianza kununua vitabu na magazeti ambavyo vilinionge zea ufahamu zaidi.

Nilitokea kupenda sana sanaa sababu ya Fema; kivipi? Jarida linatoa burudani huku likielimisha jamii hivyo nikajikuta nikipenda sana sanaa kiasi kwamba sikuona ajabu kuchagua kusomea shahada ya sanaa ili niweze kuelimisha jamii kupitia sanaa. Wapo watu wengi sana katika jamii inayonizunguka wanashangaa na kunicheka pale ninapowaambia nasomea sanaa. Binafsi najua kuna ninachokitafuta kilicho ndani ya moyo wangu, na kile wanachokisomea wao au kazi wanazozifanya wao hazitanifaa chochote katika maisha yangu. Hivyo jarida la Fema linazidi kunipa ujasiri wa kupenda sana sanaa kwani kuna burudani ndani yake.

Kimawazo, jarida limebadilisha some attitudes nilizokuwa nazo kuhusu maisha. Nilidhani kuwa pale tu nitakapomaliza Chuo nitapata kazi, lakini kwa kupitia jarida nimegundua kwamba unaweza kutopata ajira hata baada ya kuhitimu, Mfano; nimecheki story ya Benjamini Mwanambuu aliyemaliza Chuo Kikuu cha Dar es salaam toka 2005 lakini mpaka leo bado hajapata kazi ya uhakika. Hivyo jarida limeniweka tayari kukubaliana na chochote kitakachotokea mara tu baada ya kumaliza Chuo.

Ninaamini kuwa maisha yanaweza kubadilika labda kutoka hapa nilipo na kuporomoka zaidi au kutoka hapa nilipo na kupanda zaidi, mfano; Emmanuel Mgaya (Masanja) alipotoka kuwa muuza mitumba hadi kufikia kuwa msanii maarufu. Maisha yake yamebadilika kimaajabu.

Ujinsia na mahusiano ni moja ya mambo makubwa ambayo nimejifunza katika jarida la Fema. Kupitia hili jarida nimepata kuelimika na kufahamu kwa undani zaidi kuhusu ujinsia na mahusiano, hivyo elimu ninayoendelea kuipata inaniongezea ufahamu zaidi na ninaweza kuzungumzia ujinsia na mahusiano bila wasiwasi.

Ukweli kuhusu VVU/UKIMWI, kupitia jarida ambalo moja ya dhima yake kuu ni mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI. Jarida limebadilisha maisha yangu kwani nimeweza kufahamu mambo mengi yahusuyo VVU/UKIMWI. Nafahamu kwa undani kuhusu ABC's za kujikinga na VVU pia kupitia kurasa za "UKWELI KUHUSU KONDOMU" nafahamu kwa undani zaidi jinsi ya kufanya mapenzi salama. Hii imenijengea ujasiri kwani sasa naweza kumiliki kondom popote pale ninapokuwepo kama kinga dhidi ya magonjwa ya zinaa na VVU tofauti na wasichana wengine wanaodhani kwamba kitendo cha msichana kubeba kondom ni umalaya au kubeba kondom ni kazi ya mwanaume. Pale utakapotegemea mwanaume ndiyo awe nazo mnaweza kujikuta mmefanya ngono zembe kwa kuwa tu labda na yeye hakubeba kondom.

Najivunia FeminaHip Ambayo inatengeneza jarida la Fema. FeminaHip inaongoza katika usambazaji wa elimu ya mitindo bora ya maisha kwa watu wa rika zote.